MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

# Cheche za Fikra

JUZUU 5 TOLEO 16

DISEMBA 2, 2008

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!

MAKALA MAALUM

## WIZI HUU WA BOT NAO VIPI? - 1

# MEREMETA, DEEP GREEN,

## MWANANCHI GOLD NA TANGOLD



**Na. Fred Katunzi**

Mwishoni mwa juma aliyekuwa Katibu Mkuu hazina Bw. Gray Mgonja amestaafu na pamoja naye ni Katibu wa Wizara ya Ulinzi Bw. Vincent Mrisho. Hawa wawili kutokana na nafasi zao mbalimbali wanatajwa kuwemo katika mipango ya wizi mkubwa kutoka benki kuu na maamuzi ambayo yameihujumu nchi yetu mabilioni ya fedha. Tunamatumaini kuwa kustaafu kwao utakuwa ni mwanzo tu wa hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yao ili kurudisha heshima na hadhi ya utumishi wa umma tena.



Lakini pia hawa wawili wamo katika kashfa kadhaa za wizi wa Benki Kuu ambapo majina yao yamekuwa yakitajwa sana kutokana na nafasi zao.

Tunapoangalia yanayotokea kwenye sakata la EPA tunaweza kujikuta tukisahau wizi mkubwa wa Benki Kuu ambao unadaiwa kufanywa, kuongozwa na kusimamiwa na wakuu wa vyombo viwili vya Usalama (JWTZ na Usalama wa Taifa).

Tutatumia hotuba ya Mbunge wa KaratuMhe. Dr. Wilbroad Slaa (pichani) aliyoitoa Bungeni Juni 24 mwaka huu kuelezea kinagaubaga tuhuma nzito za wizi (inaendelea Uk.2-4)



Benjamin. G. Mwalukasa

### Kijarida Ulichoshika

- Kinatoka kila Jumanne
- Ni cha bure kabisa!
- Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!
- Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.
- Ni kijarida chako!
- Haki zote za kuchapa na kunakili zimeruhusiwa!

## HOJA YA MWANAKIJIJI — YA MBOMA NA APSON?

Inapofikia wakuu wa vyombo vyetu vya usalama wanatajwa kuhusika na wizi mkubwa kabisa wa fedha za Watanzania hatuna budi kuvuta pumzi kwa dakika chache na kujiuliza tumefikaje hapa.

Jenerali Robert Mboma alikuwa mkuu wa JWTZ kwa muda na Bw. Apson Mwang'onda akiwa mkuu wa Usalama wa Taifa.

Hawa wawili wanahusishwa na wizi wa mabilioni ya shilingi toka Benki Kuu mmoja kupitia Kagoda na wenzake na mwingine kupitia Meremeta.

Kinachoshangaza na kushtusha ni kuwa licha ya ushahidi mkubwa ulioko hadharani na unaojulikana hadi Bungeni watu hawa wameendelea kuwa huru na madai dhidi yao hayajapewa uzito wa wazi kuchunguzwa.

Tunaamini kuwa hata hawa wakichunguzwa na kufikishwa kizimbani, Tanzania haitalipuka. Tunataka wachunguzwe!

***Ndani ya Toleo Hili***


| | |
|---|---|
| Wizi Mkubwa BoT | 1 |
| Hoja ya Mwanakijiji | 1 |
| Wizi Mkubwa BoT | 2 |
| Wizi Mkubwa BoT | 3 |
| Wizi Mkubwa BoT | 4 |
| Gen. Mboma na Apson? | 5 |
| Picha na Katuni | 6 |

# KASHFA YA WIZI BENKI KUU

(kutoka Uk. 1)
Wa Benki Kuu.

Katika hotuba hii (ndefu kidogo) Dr. Slaa anafafanua mchakato wa wizi ulivyofanyika na anaibua maswali ambayo majibu yake tuliyakataa awali kwani ni ya kizugaji na ambayo hadi sasa hayajapatikana kwa uhakika.

Uchunguzi wa Cheche umeonesha kwa kiasi kikubwa kuwa iliposemwa kuwa "mafisadi wameiteka nchi" na ya kuwa kuwakamata wote "kutailipua nchi" kulikuwa na ukweli wa aina fulani. Ukweli kwamba wale ambao Taifa liliwaamini kulinda mali na hazina za Watanzania wao wenyewe walisimama mlangoni na kufungua mlango wa wezi kuingia huku wao wenyewe aidha wakipata malipo fulani au wakishiriki kabisa.

Ifuatayo ni hotuba ya Dr. Slaa akielezea wizi uliofanywa na makampuni makubwa manne. Hata hivyo, kinyume na mahitimisho ya Dr. Slaa kuwa fedha zilizoibwa zilitumika kwenye uchaguzi mkuu, uchunguzi wetu unaonesha kuwa ni fedha kidogo sana zilizotumika kwenye kampeni kulinganisha na fedha zilizoishia kwenye mifuko ya wakuu mbalimbali ambao baada ya kuondoka madarakani walitumia kiasi hicho cha fedha kufadhili mitaji mikubwa na kuanzisha makampuni makubwa ambayo mengine yaliweza kupata tenda nyingine za serikali!

Tunaamini kuwa fedha zilizochotwa kwa kutumia makampuni ya Mwananchi Gold, Tangold, Meremeta, na Deep Green Finance kiasi kikubwa kimeishia mifukoni na kwenye akaunti za waliowahi kuwa watumishi wa juu kabisa wa serikali na ambao leo hii wanaogopwa kutajwa kwani wavu huo utakaporushwa kukamata unaweza kukamata na waliourusha!

*Hii hapa sehemu ya Hotuba ya Dr. Slaa (tumeihariri ili kuweza kutosha katika kijarida chetu).*

Meremeta iliandikishwa Uingereza ikiwa na Hati ya Usajili na 3424504 ya Tarehe 19 August,1997 na kupata Hati ya Kutimiza Masharti (Certificate of Compliance) nchini Tanzania kama Tawi la Kampuni ya Kigeni yenye na 32755 ya tarehe 3 Oktoba, 1997.
Kinachoshangaza katika Kampuni hii ni kuwa wenye hisa wake tofauti na Bunge lilivyoelezwa mara nyingi, ni Triennex(PTY) Ltd ya Afrika Kusini yenye hisa asilimia 50%, Msajili wa Hazina mwenye hisa asilimia 50% kwa niaba ya Serikali ya Tanzania na Kampuni mbili za London Law Services Ltd wa Temple Avenue, wenye hisa 1% na London Law Secretarial Services Ltd ambao anuani yao ni sawa na hao wenzao, nao pia wana hisa 1%.


*V. Mrisho*

Hii Meremeta hasa ni ya nani, na hawa London Law Services na London Secretarial Services ni akina nani hasa. Kampuni ya Meremeta ina hisa asilimia ngapi? Haya ni mambo yanatufanya tuwe na mashaka makubwa sana. Hivi Serikali inaogopa nini kuweka mambo haya wazi hadharani, angalau kwa Kamati husika ya Bunge basi ili kama kuna sababu ya msingi wawakilishi wa Wananchi waweze kufahamu.

Vivyo hivyo kwa Kampuni ya Tangold ambayo ilisajiliwa katika cha Mauritius tarehe 05 April,2005 Ikiwa na Hati ya Usajili na 553334 na kupata Global Business Licence ( C2/ GBL) tarehe 08 April,2005. na kupata Hati ya Kutimiza Masharti hapa nchini tarehe 20 February 2006.

Hata hivyo Mhe. Spika, Taarifa zilizoko ni kuwa Tangold imekuwa na akaunti NBC Corporate Branch, no. 0111103024840 iliyofunguliwa Tarehe 1 January, 2003, yaani miaka miwili kabla Kampuni hiyo haijasajiliwa Mauritius na takriban miaka 4 tangu imepata Hati ya 'Kutimiza Masharti' Tanzania. Ni kwa vipi, kampuni hii kufanya kazi wakati Bunge lilijulishwa na Mhe. Waziri Karamagi kuwa ndiyo iliyorithi Meremeta baada ya Meremeta kufilisika?

Makampuni haya tangu yaliposajiliwa nchi za nje na hata hapa Tanzania japo yamekuwa na akaunti katika Benki za nje na za Ndani Hesabu zao hazijakaguliwa na chombo chochote hadi leo. Wahusika wa Tangold ni Bodi ya Wakurugenzi ambayo ni viongozi au waliokuwa viongozi waandamizi katika Serikali. Wakurugenzi hao ni pamoja na hayati Daudi Balali aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu (BOT), Andrew Chenge aliyekuwa Waziri wa Miundombinu, Gray Mgonja, Katibu Mkuu-Wizara ya Fedha, Patrick Rutabanzibwa- Katibu Mkuu-Maji na Vincent Mrisho-Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu.
Inakuwaje wajumbe wa Bodi ya BOT waliokuwepo wakati wote wa sakata hilo bado wamebaki katika Bodi mpya akiwemo Katibu Mkuu wa Hazina Gray Mgonja (Mgonja na Mrisho wamestaafu mwishoni mwa juma CF)

Serikali iliambie Bunge hili, ni lini uchunguzi wa kina utafanyika kuhusu ubadhirifu katika maeneo mengine yanayohusu Meremeta, Tangold, Mwananchi Gold Co. ltd na Deep Green Finance Company Ltd.?

UTATA KATI YA TANGOLD/MEREMETA NA DEEP GREEN:

Mheshimiwa Spika, kuna utata mkubwa sana kuhusu matumizi ya Fedha katika Akaunti za Tangold, Meremeta na Deep Green Finance Co. Ltd. Ili kuwapa picha kamili ya sura hii ya Ufisadi ni vema Waheshimiwa Wabunge wakaona kwa macho yao kilichotokea.

DEEP GREEN FINANCE COMPANY LIMITED

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Deep Green Finance Ltd ilianzishwa mnamo tarehe 18 Machi 2004. Kwa mujibu wa Taarifa za Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), wakurugenzi wa Deep Green Finance walikuwa ni mabwana Mark Ross Weston wa New Zealand; Anton Taljaard wa Afrika Kusini; na Rudolph van Schalkwyk pia wa Afrika Kusini.

Wote watatu ni wakazi wa Afrika Kusini na wanaelekea kuwa ni maafisa na/au wafanyakazi wa Nedbank Ltd. ya Afrika Kusini. Kufuatana na taarifa za BRELA, wanahisa wa Deep Green Finance ni mawakili Protase R.G. Ishengoma na Stella Ndikimi wa IMMMA Advocate (Waziri Lawrence Masha ni mshirika. CF); Nedbank Ltd., Nedbank Africa Investments Ltd. na SBM Nedcor Holdings Ltd. Tarehe 15 Aprili 2005 mawakili Ishengoma na Ndikimi walihamisha hisa zao kwa Nedbank Ltd. na Nedbank Africa Investments Ltd.

Taarifa za kibenki tulizonazo zinaonyesha kwamba tarehe 1 Mei 2004, Deep Green Finance ilifungua Akaunti Na. 011103024840 katika tawi la Corporate la Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Dar es Salaam. Kitu cha kushangaza ni kwamba kampuni hii iliruhusiwa kufungua na

KARIBU MWANAKIJIJI.COM

# WIZI BENKI KUU



kuendesha akaunti hiyo bila ya kuingiza hata senti moja kwa zaidi ya mwaka mmoja kuanzia tarehe "1 Mei" 2004 hadi tarehe 31 Julai 2005.

Hata hivyo kwa kipindi kifupi cha miezi minne kati ya Agosti 1 na Desemba 2005 kampuni hii ilipokea jumla ya shilingi 10,484,005,815.39 kutoka Wizara ya Fedha na/au BOT bila kuonyesha wazi ni biashara gani Kampuni hii imefanya na Wizara ya Fedha au BOT. Fedha hizo zilitolewa kwa utaratibu ufuatao:

(a) Tarehe 1 Agosti 2005 BOT, kwa kutumia hundi Na. 241740, ilihamisha dola za Marekani 1,354,167.26 au shilingi za Tanzania 1,546,778,770.92 kwenda kwenye akaunti ya Deep Green Finance. Siku hiyo hiyo fedha hizo zote zilitolewa kwenye akaunti ya Deep Green Finance kwa utaratibu maalum wa haraka (special clearance) na katika cash kwa Fedha za Tanzania japo zilipelekwa katika Dola za Marekani, jambo linalotia shaka kuhusu malengo ya fedha hizi, hasa ikizingatiwa kuwa waliochukua ni Wageni.

(b) Tarehe 1 Septemba 2005 BOT, kwa kutumia hundi Na. 015558, ilihamisha dola za Marekani 1,827,137.44 au shilingi za Tanzania 2,083,255,881.60 kwenda kwenye akaunti ya Deep Green Finance. Siku hiyo hiyo jumla ya shilingi 2,083,333,333.33 zilitolewa kwa mara nyingine tena kwa kutumia utaratibu maalum wa haraka tena kwa cash;

(c) Tarehe 8 Septemba 2005 Tangold Ltd ilihamisha dola za Marekani 100,256.62 au shilingi za Tanzania 114,611,746.80 kwenda kwenye akaunti ya Deep Green Finance. Itakumbukwa kwamba Tangold Ltd. ni kampuni ya kigeni iliyoandikishwa nchini Mauritius tarehe 5 Aprili 2005 na kupewa Cheti cha Kutimiza masharti ya Tanzania tarehe 20 Februari 2006. Wakurugenzi wa Tangold Ltd. Ni wale ambao tulikwisha kuwataja huko nyuma. Kufuatana na barua ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa BOT ya tarehe 21 Desemba 2006, Tangold Ltd. ililipwa na BOT dola za Marekani 13,736,628.73 kwa kupitia akaunti isiyojulikana ya Nedbank Ltd. ya Afrika Kusini na kwa madhumuni yasiyojulikana;

(d) Tarehe 16 Septemba 2005 jumla ya shilingi 129,000,000.00 zilitolewa kutoka kwenye akaunti ya Deep Green Finance na kuwekwa kwenye akaunti ya muda maalum (FDR);

(e) Tarehe 3 Oktoba 2005 hundi ya BOT Na. 16596 yenye jumla ya shilingi 2,083,333,333.33 za Wizara ya Fedha ililipwa kwa utaratibu maalum wa haraka kutoka kwenye akaunti ya Deep Green Finance. Inaelekea hundi hiyo ililipwa kabla fedha hazijaingizwa kwenye akaunti ya Deep Green Finance kwa vile tarehe 4 Oktoba 2005 BOT ilihamisha dola za Marekani 1,789,075.89 au shilingi 2,083,891,765.35 kwenda kwenye akaunti ya Deep Green Finance;

(f) Tarehe 8 Oktoba 2005 jumla ya shilingi 39,761,397.98 zilihamishwa kutoka kwenye akaunti ya Deep Green Finance kwenda Tangold Ltd.;

(g) Tarehe 31 Oktoba 2005 jumla ya shilingi za Tanzania 2,083,333,333.33 fedha za Wizara ya Fedha zilihamishiwa kwenye akaunti ya Deep Green Finance kwenda kusikojulikana;
(h) Tarehe 2 Novemba 2005 dola za Marekani 1,821,095.57 au shilingi za Tanzania 2,083,653,279.68 zilihamishwa kutoka kwenye akaunti ya Deep Green Finance kwenda kusikojulikana;

(i) Tarehe 30 Novemba 2005 BOT ilihamisha shilingi za Tanzania 2,083,333,333.33 fedha za Wizara ya Fedha kwenda kwenye akaunti ya Deep Green Finance. Siku moja baadaye, dola za Marekani 1,817,199.52 au shilingi za Tanzania 2,184,610,383.04 zilihamishwa kutoka kwenye akaunti ya Deep Green Finance kwenda kusikojulikana;

(j) Tarehe 10 Desemba 2005 shilingi 100,940,489.71 zilihamishwa kutoka Tangold Ltd. kwenda kwenye akaunti ya Deep Green Finance. Hii ilikuwa ni siku nne tu kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Desemba 14, 2005 kufanyika nchini kote;

(k) Tarehe 19 Desemba 2005, siku tano baada ya Uchaguzi Mkuu kufanyika, dola za Marekani 88,722.17 au shilingi za Tanzania 104,755,554.09 zilihamishwa kutoka kwenye akaunti ya Deep Green Finance kwenda kusikojulikana;

(l) Tarehe 9 Februari 2006 shilingi 3,836,800.00 zilihamishwa kwenda akaunti ya mawakili wa Deep Green Finance, IMMMA Advocates, iliyoko benki ya Standard Chartered. Haijulikani kama fedha hizi zilikuwa ni kwa ajili ya malipo ya mawakili hao au la;

(m) Malipo ya mwisho kutoka kwenye akaunti ya Deep Green Finance yalifanywa tarehe 22 Novemba 2006 ambapo jumla ya shilingi 14,465,000.00 zilihamishiwa katika akaunti isiyojulikana ya benki ya Standard Chartered na kwa matumizi yasiyojulikana;

Kutokana na rekodi za kibenki zilizoonyeshwa hapo juu, jumla ya shilingi 10,484,005,815.39 ziliingizwa katika akaunti ya Deep Green Finance katika kipindi cha miezi minne tu kati ya tarehe 1 Agosti na 10 Desemba 2005. Hiki kilikuwa ni kipindi cha mchakato na/au kampeni za Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 14 Desemba 2005. Aidha, kuanzia tarehe 11 Desemba 2005 hakuna fedha yoyote iliyoingizwa katika akaunti hiyo hadi tarehe 27 Februari 2007 kampuni hiyo ilipovunjwa 'kwa hiari' ya wanahisa wake.



*Gray Mgonja*

Ni muhimu kurudia kwamba, kwa ushahidi huu wa nyaraka za kibenki, kampuni ya Deep Green Finance haikuwa na hata senti moja kabla ya tarehe 1 Agosti 2005 na wala haikupokea hata senti tano baada ya tarehe 10 Desemba 2005 . Mheshimiwa Spika, kwa mtu yeyote makini ni lazima kupata tafsiri sahihi ya mchakato huu.

Kwa taarifa za sasa hivi, inafahamika kwamba faili la Deep Green Finance lililotakiwa kuwa BRELA limetoweka, isipokuwa Hati ya Kufunga Kampuni (Winding Up). Tuna kila sababu ya kuamini kwamba hii ilikuwa ni kampuni hewa (shell company) iliyoundwa kwa ajili tu ya kupitishia fedha za umma kutoka Benki Kuu kwenda kwenye kampeni za Uchaguzi Mkuu wa 2005.

TANGOLD LIMITED

Kampuni hiyo ilipewa hati ya kutimiza masharti ya Tanzania tarehe 20 Februari 2006, nyaraka za kibenki tulizonazo zinaonyesha kwamba Tangold Ltd. ilifungua akaunti ya shilingi Na. 011103024852 NBC Corporate Branch tarehe "1 Januari 2003". Kama ilivyokuwa kwa Deep Green Finance, siku ya TANGOLD kufungua akaunti yake

Soma bure

# MEREMETA, DEEP GREEN, MWANANCHI NA TANGOLD!

ilikuwa ni siku ya Mwaka Mpya na hiyo ni siku ya Mapumziko dunia nzima.

Taratibu za kibenki za ufunguaji wa makampuni zinalazimu kampuni husika kuwasilisha benki nakala ya usajili, nakala ya Katiba kabla ya kuruhusiwa kufungua Akaunti, na hati ya Mlipa Kodi ( registration certificate). Taratibu za kibenki za ufunguaji wa akaunti za makampuni zinalazimu kampuni husika kuwasilisha benki nakala ya usajili wa kampuni na Katiba yake kabla ya kuruhusiwa kufungua akaunti.

Swali la kujibiwa na NBC pamoja na watawala wa nchi hii ni je, ilikuwaje Tangold Ltd. waliruhusiwa kufungua na kuendesha akaunti ya benki kabla hawajaandikishwa nchini Mauritius achilia mbali kupata hati ya kutimiza masharti ya Tanzania? Kifungu cha 7 cha Memorandum and Articles of Association kinataja wazi kuwa wenye hisa wanaweza kuhamisha hisa zao kwa Baba, mke, mtoto na mpwa.

Bunge hili lielezwe Kama kweli TANGOLD ni mali ya Serikali kwa asilimia mia moja, Baba, mke ,mtoto, na mpwa wa Serikali ni nani?

Pili, kampuni ya Tangold Ltd, iliendesha akaunti hiyo bila kuweka au kutoa fedha yoyote ile kati ya tarehe 1 Januari 2003 hadi tarehe 1 Agosti 2005 ilipoanza kunyeshewa mvua ya neema ya mabilioni ya fedha za walipa kodi wa Tanzania kutoka BOT! Mvua hiyo ni nje ya mvua ya dola za Marekani 13,340,168.37 iliyohojiwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali na iliinyeshea Tangold Ltd. kama ifuatavyo:

(a) Tarehe 1 Agosti 2005 BOT ilihamisha shilingi za Tanzania 4,703,221,229.08 kwenda kwenye akaunti ya Tangold Ltd.; Tarehe hii ni muhimu sana kwani ndiyo siku ambayo BOT ilifanya pia malipo ya kwanza kwa Deep Green Finance kama ilivyoelezwa katika Taarifa hii. Ukijumlisha kiasi hiki na kile kilichohamishwa kwenye akaunti ya Deep Green ni jumla ya Tshs 6.2 Billion. Fedha zote hizi zilichukuliwa kwa 'cash'. Inashangaza waliozichukua fedha hizi walizebebaje kwani wataalam wanakisia kuwa sawa na Tani 50 zinazoweza kubebwa na kubebwa tu na lori 5 za Tani 10 kila moja? Hili linabaki kuwa fumbo.

(b) Tarehe 2 Septemba 2005 Tangold Ltd. ilihamisha shilingi za Tanzania 244,428,386.15 kutoka akaunti yake hiyo kwenda kwenye akaunti ya Deep Green Finance; Kama tulivyoelezea katika Taarifa hii Deep Green Finance ililipwa tarehe 1 Augusti, 2005, Tshs 2,083,255,881.60 na BOT.

(c) Tarehe 8 Oktoba 2005 shilingi za Tanzania 39,761,397.98 zilihamishiwa kwenye akaunti ya Tangold Limited kutoka kwenye akaunti ya Deep Green Finance;



(d) Tarehe 12 Oktoba 2005 Tangold Ltd. ilihamisha shilingi za Tanzania 1,690,500,000.00 kwenda Meremeta Limited;

(e) Tarehe 23 Novemba 2005 Tangold Ltd. ilihamisha shilingi za Tanzania 555,300,048.00 kwenda Meremeta Ltd.;

(f) Tarehe 10 Desemba 2005 Tangold Ltd. ilihamisha shilingi za Tanzania 100,940,489.71 kwenda kwenye akaunti ya Deep Green Finance;

(g) Tarehe 12 Desemba 2005, siku mbili kabla ya Uchaguzi Mkuu, Tangold Ltd. ilihamisha shilingi za Tanzania 551,060,000.00 kwenda kwenye akaunti ya Meremeta Ltd.

Baada ya hapo Tangold Ltd. haikupokea wala kuingiza fedha zozote kwenye akaunti yake hadi tarehe 6 Juni 2006. Tangu tarehe hiyo hadi leo hii Tangold Ltd. haijaweka wala kutoa fedha nyingine yoyote katika akaunti hiyo. Kwa maana hiyo, katika kipindi cha miezi minne Tangold Ltd. iliingiziwa na BOT jumla ya shilingi za Tanzania 4,742,982,627.06 na ilifanya malipo kwa Deep Green Finance na Meremeta Ltd. ya jumla ya shilingi za Tanzania 3,363,531,259.67.

Mheshimiwa Spika, maswali muhimu ya kujiuliza kuhusiana na Tangold Ltd. ni haya yafuatayo. Kwanza, ilikuwaje kampuni ambayo haikuwa hata imeandikishwa kisheria ikalipwa mabilioni ya fedha za walipa kodi na/au ya umma na bila maelezo yoyote?
Pili, ilikuwaje Serikali, kupitia kwa aliyekuwa Waziri Karamagi, itoe taarifa ya uongo Bungeni kwamba Tangold Ltd. ni kampuni mpya na imeanzishwa ili kurithi mali na madeni ya Meremeta Ltd. wakati makampuni yote mawili yalikuwa yakipeana mabilioni ya fedha za umma wakati wa mchakato wa Uchaguzi Mkuu katika mazingira ya kutatanisha?

Tatu, kwa nini malipo ya mabilioni haya yalikoma mara baada ya Uchaguzi Mkuu ?

Tuhuma hizi nzito zinaihusisha moja kwa moja Serikali na watendaji wake wakuu kutokana na mfumo huu wa kuhamisha fedha za umma (transaction) bila maelezo ya kutosha. Aidha tunawaomba wananchi wa Tanzania wenye mapenzi mema na Taifa letu waidai Serikali iwaeleze mabilioni haya yalilipwa kwa ajili gani.
kwamba tarehe 1 Mei 2004, Deep Green Finance ilifungua Akaunti Na. 011103024840 katika tawi la Corporate la Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Dar es Salaam. Kitu cha kushangaza ni kwamba kampuni hii iliruhusiwa kufungua na kuendesha akaunti hiyo bila ya kuingiza hata senti moja kwa zaidi ya mwaka mmoja kuanzia tarehe "1 Mei" 2004 hadi tarehe 31 Julai 2005.
Hata hivyo kwa kipindi kifupi cha miezi minne kati ya Agosti 1 na Desemba 2005 kampuni hii ilipokea jumla ya shilingi 10,484,005,815.39 kutoka Wizara ya Fedha na/au BOT bila kuonyesha wazi ni biashara gani Kampuni hii imefanya na Wizara ya Fedha au BOT. Fedha hizo zilitolewa kwa utaratibu ufuatao:

(a) Tarehe 1 Agosti 2005 BOT, kwa kutumia hundi Na. 241740, ilihamisha dola za Marekani 1,354,167.26 au shilingi za Tanzania 1,546,778,770.92 kwenda kwenye akaunti ya Deep Green Finance. **(itaendelea wiki ijayo)**

**KARIBU MWANAKIJIJI.COM**

HOJA YA NGUVU

# KASHFA BOT: APSON NA GEN. MBOMA?

Na. Ben Mwalukasa

**(Makala ya "Vitu vya Lazima" itaendelea wiki ijayo)_**

Aliyekuwa Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa Bw. Apson Mwang'onda na aliyekuwa Mkuu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania Jenerali Mstaafu Robert Mboma (pichani) wamejikuta wakianza kuzungukwa na wingu kubwa la kashfa kufuatia majina yao kutajwa na vyanzo mbalimbali kuwa ndiyo wahusika wa makampuni makubwa ambayo yanatuhumiwa kuchota mabilioni ya fedha kutoka Benki Kuu ya Tanzania kati ya mwaka 2005 na 2006.



Bw. Mwang'onda anatajwa katika kampuni ya Kagoda na pia kuhusishwa na ukimya wa Usalama wa Taifa wakati wizi mkubwa unatokea Benki Kuu.

Jenerali Mboma kwa upande wake anatajwa kuhusika na kampuni ya "Jeshi" ya Meremeta katika wizi mwingine ambao unajulikana kutokea Benki Kuu ambapo kampuni hiyo ilichotewa mabilioni mengi katika mazingira ya kushangaza, mazingira ambayo hata Wabunge wamejikuta wakishindwa kupata majibu ya uhakika.

Kama ilivyooneshwa kwenye hotuba ya Dr. Slaa kampuni ya Meremeta imekuwa na utata wa kushangaza na majibu ambayo yamekuwa yakitolewa mara kwa mara yamekuwa yakichanganya umma na ambayo kwa mtu yeyote mwenye utimamu wa mawazo atagundua kuwa kuna kitu kinafichwa.

Mojawapo ya mambo ya kushangaza ni kuwa Kampuni hii mwanzoni tuliambiwa ni ya Jeshi lakini jinsi mambo yake yalivyoishia imeonekana ni kampuni ya binafsi. Lakini baadaye aliyekuwa Mkuu wa Jeshi letu Gen. Robert Mboma anatajwa kuwa alikuwa ni Mkurugenzi wa kampuni hiyo.

Baadaye ilidaiwa Bungeni na Mhe. John Cheyo (Bariadi Mashariki- UDP) kuwa kulikuwa na "Meremeta" mbili yaani ile iliyokuwa kweli mali ya serikali na baadaye ile iliyogeuzwa kuwa ya watu binafsi. Kwa mujibu wa gazeti la Raia Mwema "Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali (CAG), Ludovick Utouh, imetamka bayana kwamba haijawahi kukagua hesabu za Meremeta Gold, na kampuni hiyo tata inaelekea haimo katika orodha ya makampuni yanayomilikiwa na Serikali ama kwamba Serikali ina hisa katika kampuni hiyo." (Toleo la 038, Julai 16, 2008).

Kampuni hiyo ya Meremeta ambayo hadi leo serikali "haijui" mmiliki wake hasa ni nani na kwanini ililipwa mabilioni ya shilingi na baadaye kufilisiwa inapohushishwa na shughuli binafsi za aliyekuwa Mkuu wa Jeshi hatuna budi kujiuliza imekuwaje?

Wakati huo huo aliyekuwa Mkuu wa Usalama wa Taifa Bw. Apson Mwang'onda anahusishwa na kushiriki katika mipango ya utekelezaji wa upotevu wa fedha za EPA. Zaidi ya yote yeye mwenyewe na watu wake wa karibu wanatajwa kuhusika na Kagoda. Zaidi ya yote yeye naye kama Mboma alipotoka katika wadhifa wake akaaingia kwenye shughuli zake za biashara na kuwa na ushirika wa biashara na kampuni moja ya Teknolojia ya Mawasiliano ambayo kwa namna ya ajabu ikapata tenda za kutoa huduma za vifaa vya mawasiliano hadi Ikulu na pia kutaka kupewa nafasi ya kuhusishwa na mambo ya Usalama wa Benki Kuu na ujenzi wa Benki Kuu Zanzibar.

> ***Wanachodaiwa kufanya kama siyo uhaini basi kinapakana nacho!***

Lakini hawa watu wawili hadi hivi sasa hakuna dalili yoyote ya kuwagusa inayoonekana na bila ya shaka ndio wanaleta hofu ya kufanya nchi ionekane kama imetekwa nyara. Endapo kwa namna yeyote ile viongozi hawa kweli wamehusika na kujipatia fedha wao wenyewe au kuwafungulia watu wengine milango ya hazina zetu, walichokifanya ni zaidi ya usaliti wa mtu kwa nchi yake bali ni uhalifu mkubwa zaidi dhidi ya Jamhuri yetu.

Tunatoa wito kwa uchunguzi huru kufanyika (siyo wa DPP) na kuomba vyombo vya kimataifa kufanya uchunguzi huo na kuwafuatilia wale wote wanaohusika na makampuni mengine yote yanayohusiana kuchota fedha za wananchi kutoka Benki Kuu.




Wakati fedha za EPA zilikuwa ni za malimbikizo ya madeni ya nje (kwa makampuni mbalimbali) fedha zilizokwenda kwa Deep Green Finance, Mwananchi Gold, Meremeta, na Tangold ni fedha za walipa kodi wa Tanzania. Baadhi yake ni fedha za misaada mbalimbali zinazotolewa na wafadhili. Kiasi kilichokombwa toka benki yetu Kuu kingewea kufanya mambo makubwa kabisa.

Ni lazima wahusika wote watafutwe, wachunguzwe na wawajishwe kwa nguvu zote za sheria. Kama kuna wakati tunahitaji msaada wa mataifa ya kigeni, msaada wenye maana ni katika kuwachunguza watu hawa.

Watumishi waliopewa dhamana ya kulinda usalama wa Taifa letu na hazina zetu na wale waliopewa madaraka kutuongoza wanapohusishwa na tuhuma za ufisadi jambo hilo si la mzaha hata kidogo. Na kama kweli watu hao wametumia nafasi zao kujipatia mitaji ya miradi yao, na kujinufaisha wao na watoto wao, wanachofanya kwa hakika ni kutusaliti sisi wananchi, na kutufanya tuwe wageni katika nchi yetu. Kitendo chao kama sio cha kihaini basi kinapakana na kosa hilo.

Yawezekana hii ndiyo sababu kubwa kumekuwa na kusita sita katika kushughulikia jambo hili kwani yawezekana likagusa mambo mengi na watu wengi kweli.

Ni kwa sababu hiyo tunapinga vikali kitendo cha Bw. Elisifa Ngowi ambaye anatajwa kwenye mojawapo ya makampuni yaliyochota EPA kuhusishwa katika kuongoza kamata kamata hii kama Mtumishi wa Usalama wa Taifa. Haiwezekani mmoja wa watuhumiwa awe kwenye uchunguzi!

**MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...**

## Picha za Wiki



Watuhumiwa: Daniel Yona (kushoto) (CCM) na Mhe. Basil Mramba (Rombo—CCM)

**PATA HABARI MOTOMOTO NA MIJADALA**

**http://www.mwanakijiji.com**

**Jiandikishe kushiriki mijadala, kupata habari, kusikiliza muziki masaa 24 na matangazo ya moja kwa moja kila mwishoni mwa juma**.

Ukizungumzia habari, unatuzungumzia sisi!

# KATUNI ZA WIKI







## KUTOKA KWENYE MTANDAO

**Elisifa Ngowi**—Mmiliki wa Clayton Marketing Limited . Kampuni hiyo iliandikishwa Juni 2005 na inamtaja Bw. Ngowi na Edwin Mtoi kama Wakurugenzi na wanahisa pekee. Kampuni hiyo Kitalu Na.707 mtaa wa wa Mkwepu jijini Dar es Salaam.

Pia Bw. Ngowi anatajwa kama ni mmoja wa wanahisa wa kampuni ya Excellent Services Ltd ambayo iliandikishwa mwaka 1992. Pamoja naye ni Emily Samanya, Peter Sabas, Lecis Msiko and Massimo Faneli. Anuani yake kampuni hiyo ni Kitalu Na.11649 Sokoine Drive, kwanini huyo huyo ameitwa baada ya kustaafu kuongoza kampeni dhidi ya "wenzake"? - **Nzi wa KLHN**

Ni kashfa kubwa kwa waziri kufanya lobbying na mahabusu kwa lengo la kutaka wapate upendeleo wa aina yoyote kwa sababu tu eti ni marafiki zake...hii inahatarisha utawala wa kisheria na kupunguza imani waliyo nayo wananchi kwa mihili ya utawala yaani, serikali na mahakama bila kulizungumzia bunge hapa! - **Jingo**

kwani mtu akiwa fisadi ndo hana marafiki? watu tunapendana wakati wa sida na raha hata kama ni kiongozi ana haki yake kama wengine walivyo na haki jamani tusiwakandamize sana,hata majambazi wana marafiki na marafiki si lazima wawe majambazi wenzao—**Naka**

Bado wengine hawajakamatwa na mmoja wapo ni John Pombe Magufuli,nyumba za serikali,barabara ya biharamulo na bomoabomoa ikiwemo kituo cha Mafuta Mwanza kilichoigharimu serikali mabilioni ya pesa. - **Sinajina**

Mimi kwanza nakupongeza mwanakijiji kwani wewe ulianza kutuhabarisha hii ishu kabla hata ya wiki moja na kweli ulivyosema Mramba anasubiriwa amuage mtoto wake ktk send off wiki iliyopita, hivyo basi kweli habari zako ni za ukweli na uhakika! - **Mjuba**

**CHAPA NA MPATIE MTU MWINGINE BURE**


## Cheche za Fikra

Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi

Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha, maoni, habari, na ushauri

Tuandikie: Mhariri@klhnews.com

Tovuti: http://www.mwanakijiji.com



***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*